JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA



# JARIDA LA RS RUVUMA
## TOLEO LA PILI MEI 2024



*RC Ruvuma afungua masoko ya ufuta,soya na mbaazi* UK. 10




*Timu ya Tulia Trust yabisha hodi Ruvuma* UK.13





## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA PILI MWEZI MEI 2024

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

# YALIYOMO

1.Mwenge wa Uhuru kuanza mbio zake Ruvuma Juni 8
2.Viazi mviringo kuanza kulimwa Ruvuma-utafiti
3.Mwambesi hifadhi ya asili yenye ndege adimu Duniani
4.Bado vijiji 16 tu Ruvuma kufikishiwa umeme
5.RC Ruvuma afungua masoko ya ufuta,soya na mbaazi
6.Uzalishaji mazao Ruvuma wafikia tani milioni 1.8
7.Watumishi wa umma Nyasa wapata mafunzo ya PEPMIS
8.Timu ya Tulia Trust yabisha hodi Ruvuma
9.Serikali yatoa bilioni 9.34 kujenga vituo vya afya 14 Ruvuma
10.Mbinga yatinga kumi bora mashindano ya usafi
11.Rais Samia alivyoboresha miundombinu Ruvuma
12.Uzalishaji parachichi Mbinga wafikia asilimia 400
13.TAMCU yapata viongozi wapya,DC Tunduru atoa maagizo
14.Madaba wapongezwa kwa kufanya vizuri mitihani ya Taifa
15.DED Songea aagiza kasi utekelezaji miradi ya maendeleo
16.RC Ruvuma atahadharisha shughuli za kiuchumi zisizofuata sheria
17.Shirika la BRITEN latoa elimu ya viuatilifu kwa wakulima Madaba
18.DED Mbinga awafunda wanafunzi
19.BODI ya VETA yafanya ziara Ruvuma
20.Mkuu wa Mkoa awapongeza wasanii wa Nyota ya Ruvuma
21.FORVAC yakabidhi mashine kuchakata magogo Songea
22.Serikali kutoa maamuzi soko la madini ya vito Tunduru
23.RC Ruvuma asikitishwa na hali ya malezi ya watoto
24.Wagonjwa 568 Madaba wapata huduma za kibingwa
25.Luteni Kanali aliyesoma na Idd Amini alivyozikwa kijeshi Songea
26.Ruvuma walivyoadhimisha siku ya Mama Duniani
27.Mbunge Nyasa atoa kilo 500 za mchele Lituhi
28.DC Tunduru aagiza usimamizi chakula shuleni
29.Wanafunzi Madaba kupima uoni na usikivu
30.DAS Songea aeleza umuhimu wa chakula cha mchana kwa wanafunzi

## TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.
Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## KARIBU MWENGE WA UHURU MKOANI RUVUMA



MWENGE wa Uhuru unatarajia kuanza mbio zake mkoani Ruvuma kuanzia Juni 8 na kukamilisha mbio zake Juni 15,2024.

Kwa mujibu wa ratiba ya Mwenge wa Uhuru 2024,Mwenge wa Uhuru utapokewa mkoani Ruvuma ukitokea mkoani Mtwara Juni 8,2024 katika Kijiji cha Sautimoja wilayani Tunduru.

Kulingana na ratiba hiyo Mwenge wa Uhuru,Juni 8 utakimbizwa katika Halmashauri ya Tunduru,Juni 9 Namtumbo,Juni 10 Halmashauri ya Songea,Juni 11 Halmashauri ya Mbinga,Juni 12 Nyasa,Juni 13 Halmashauri ya Mbinga Mji,Juni 14 Songea Manispaa na Juni 15 Halmashauri ya Madaba.

Mwenge wa Uhuru unatarajia kukabidhiwa katika Kijiji cha Mavanga wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe Juni 16,2024.

Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni ***tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu***

## VIAZI MVIRINGO KUANZA KULIMWA MKOANI RUVUMA



UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini (SAGCOT) katika Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma kuanzia mwaka 2020 hadi 2024 umebaini kuwa viazi mviringo vimetoa matokeo mazuri katika uzalishaji.

Afisa Kilimo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Onesmo Mpuya akizungumza kwenye zoezi la kuzindua uvunaji wa zao la viazi mviringo katika shamba darasa la majaribio Kata ya Tanga Manispaa ya Songea ya Songea, amesema SAGCOT wamefanya utafiti wa kulima viazi mviringo katika vijiji vya Liganga,Mang'ua na Tanga wilayani Songea na zao hilo kuonesha mafanikio makubwa katika uzalishaji.

"Watu wengi wanaamini viazi mviringo vinastawi vizuri mkoani Njombe na hata mimi nilikuwa naamini hivyo,kumbe kama huna utafiti huna haki ya kusema,utafiti wetu wilayani Songea umebaini viazi mviringo vinafanya vizuri sana'',alisisitiza Mpuya.

Ametoa rai kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kuona fursa ya kutengeneza uchumi na kuongeza kipato kupitia zao la viazi mviringo ambapo utafiti umebaini kuwa heka moja ya viazi mviringo inazalisha magunia 200 hivyo kumuingizia mkulima wastani wa shilingi milioni 16.

Amesema Idara ya kilimo Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na SAGCOT inahamasisha kilimo cha parachichi katika Mkoa wa Ruvuma ambapo hadi sasa kuna Zaidi ya hekari 500 ambazo zimepandwa parachichi ambazo ambazo huanza kuzaa baada ya miaka mitatu.

Mgeni rasmi kwenye hafla ya uvunaji viazi mviringo,Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Mheshimiwa Michael Mbano amesema wakulima wa Songea kwa muda mrefu wamekuwa wakitegemea zao moja la mahindi ambapo amesema zao la parachichi na viazi mviringo linakwenda kuleta fursa mpya na tija kwa wakulima.

Mbano amesisitiza kuwa wakati anapata taarifa za uzinduzi uvunaji viazi mviringo hakuamini kama ardhi ya Songea inafaa kwa kilimo cha zao hilo na kwamba wananchi wengi wa Songea hawana taarifa kama viazi mviringo vinaweza kustawi na kuwaongezea kipato.

Amesema tani 20 za viazi mviringo ambazo zinavunwa kwa hekari moja ni uchumi ambao kila mwananchi wa Mkoa wa Ruvuma anatamani kupata ambapo pia ametoa rai kwa wananchi wa Songea kulima zao la parachichi ambalo pia linatoa kipato kikubwa

Amesema utafiti umebaini mti mmoja wa parachichi kwa mwaka unaweza kumuingia mkulima kati ya shilingi 500,000 hadi 800,000 hivyo ametoa rai kwa wananchi wa Manispaa ya Songea kupanda miti ya matunda kama parachichi na viazi mviringo ili kukuza uchumi wao.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima cha LUSITU AGRI BUSSINESS ambaye pia ni Mkulima Mwezeshaji Beno Mgaya ameitaja Taasisi ya Kuendeleza

Kilimo Nyanda za Juu Kusini (SAGCOT) imedhamiria kutoa mafunzo ya kilimo biashara ili wakulima waweze kujitambua kwa kuhamasisha kilimo cha parachichi na viazi mviringo katika Mkoa wa Ruvuma.

Amesema utafiti walioufanya katika wilaya ya Songea kuhusu zao la viazi mviringo kwa kutumia mbegu za aina mbili kutoka nchini Uholanzi zimetoa matokeo mazuri na kwamba hapa nchini hivi sasa kuna aina 16 za mbegu za viazi mviringo.

Mgaya amelitaja lengo la kuanzisha kilimo cha viazi mviringo ni kumwezesha mkulima kupata kipato wakati anasubiri zao la parachichi ambalo huchukua miaka mitatu hadi kuanza kuzaa mkoani Ruvuma.

Amesema SAGCOT imedhamiria kuwa na mashamba darasa katika zao la viazi mviringo katika maeneo ya Shule ya Tanga, Liganga,Litapwasi,Namatuhi na Peramiho wilayani Songea na kwamba mashamba darasa yote yapo katika mfumo wa umwagiliaji.

Hata hivyo amesema wakulima wa viazi mviringo mkoani Ruvuma wataweza kuzalisha kwa kutumia umwagiliaji hivyo kuzalisha mwaka mzima na kumwezesha mkulima kupata kipato kizuri Zaidi.

Mwenyekiti huyo anamshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuiamini SAGCOT ili iweze kufanya kazi Tanzania nzima ambapo hadi sasa imeenea katika mikoa tisa.



Baadhi ya viazi mviringo ambavyo vimevwa katika shamba darasa la Shule ya Tanga Manispaa ya Songea

# MWAMBESI MSITU WA HIFADHI WENYE NDEGE ADIMU DUNIANI




MSITU wa Hifadhi wa Taifa wa mazingira asilia Mwambesi uliopo wilayani Tunduru mkoani Ruvuma ulianzishwa mwaka 1956 na ulipandishwa hadhi kuwa msitu wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2017/2018.

Meneja wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Denis Mwangama katika wilaya ya Tunduru anasema msitu huo umepandishwa hadhi ili kuongeza uhifadhi zaidi kutokana na kuwa na utajiri wa viumbe vya kipekee duniani wakiwemo wanyama,ndege na mimea.

Anawataja wanyama waliopo katika msitu huo ambao upo kando kando mwa Mto Ruvuma kuwa ni simba, tembo, chuo,kuro,jamii za nyani,jamii za swala,nyati na wanyama wengine.

Mwangama anasema Katika msitu wa Mwambesi kuna jamii ya ndege maarufu duniani anayeitwa Pentiole ambaye utafiti uliofanywa na PALMS Foundation mwaka 2015 umebaini kuwa ndege huyo amehamia kutoka nchini Madagaska baada ya mazingira aliyokuwa anaishi kuharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Kwa mujibu wa Mwangama, ndege huyo ana tabia ya kuzamia samaki kutoka majini na kwamba ndege hao wanapenda kuishi kwenye maporomoko ya Mto Ruvuma yanayoitwa Sunda ambayo yapo ndani ya hifadhi hiyo.

“Tanzania tuna bahati katika msitu wetu tuna ndege Pentiole ambaye amekuwa akiishi ukingoni mwa maporomoko ya maji yajulikanayo kama Sunda Water falls’’,anasisitiza.

Kwa mujibu wa Mwangama Ndege huyu huogolea kulingana na mawimbi ya maji yadondokayo kwenye maporomoko hayo akitatafuta mawindo yake ya samaki maana ndicho chakula chake pekee.

Licha ya ndege huyo Mwangama anayataja maporomoko ya Sunda kuwa ni miongoni mwa vivutio vya utalii katika hifadhi ya Mwambesi na kwamba maporomoko hayo yalitumika wakati wa vita ya Majimaji kati ya mwaka 1905 hadi 1907 ili kujificha kwenye mapango kwa juu.

Mto huu ndio uliokuwa ukitumika kwenye vita vya Majimaji ambapo watu wa makabila ya Ukanda wa Kusini hususani Wangoni walitumia maji yake katika kuzimia silaha za moto chini ya uongozi wa Kinjeketile Ngwale.

Pia eneo hilo linaaminika Wajerumani walitumia kama njia kubwa wakitokea Msumbiji katika biashara ya meno ya Tembo na Waarabu walipita pembezoni mwa mto huo kuwapitishia watumwa.

Hata hivyo anasema awali kabla ya serikali kuamua msitu huo kuwa Msitu wa hifadhi,kulikuwa na vitalu vya uwindaji wa kitalii ambapo ndani ya msitu kulikuwa na kambi ya wawindaji iliyoitwa Big Game ambayo ilikuwa na Kampuni ya uwindaji iliyoitwa Tandara Hunting Safaris.

Kulingana na Meneja huyo,msitu huo una ukubwa wa zaidi ya hekta 112,000 na kwamba umbali toka Tunduru mjini hadi ofisi za msitu huo ni kilometa 90.

“Msitu huu upo kando kando mwa Mto Ruvuma ambao pia unafanya mpaka wa asili kwa upande wa kusini magharibi mwa msitu,kupitia mto Ruvuma kuna fukwe nzuri ambazo ni kivutio kwa wageni wanapotembelea msitu huu ’’,anasema.

Meneja huyo wa TFS anasema Hifadhi ya Mwambesi pia ina wanyama wa mtoni kama mamba na viboko ambapo wakati wa masika wanakuwa wengi na kuvutia wageni wanaobahatika kutembelea msitu huo.

Anasema mtalii akiwa katika msitu wa Mwambesi anaweza kufanya utalii wa kuteleza kwenye mitumbwi katika Mto Ruvuma.

Deborah Mwakanosya ni Meneja wa Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Mazingira Asilia Mwambesi anasema Mwambesi ni msitu wa asili wa pili kwa ukubwa kwa Tanzania ukiongozwa na msitu wa Kilombero mkoani Morogoro.

Anasema msitu huo ambao umezungukwa na Mto Ruvuma, umesheheni baianowai mbalimbali za mimea adimu duniani ikiwemo miti aina ya mipozipozi ambayo ina tabia ya kudondosha maji,miti hiyo inapatikana sehemu chache duniani ukiwemo msitu wa Mwambesi.

## BADO VIJIJI 16 TU RUVUMA KUFIKISHIWA HUDUMA YA UMEME




VIJIJI vinavyopata umeme katika Mkoa wa Ruvuma vimeongezeka kutoka vijiji 489 mwezi Machi 2024 Hadi kufikia vijiji 538 mwezi Mei 2024.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Ruvuma Eliseus Mhelela amesema ongezeko hilo linatokana na kazi zinazofanywa na wakandarasi walioko katika vijiji mbalimbali mkoani Ruvuma.

Mhelela amesema mpaka kufikia Machi 2024 vijiji vilivyopata umeme vilikuwa 489 sawa na asilimia.88.3 ya vijiji vyote 554 vya Mkoa wa Ruvuma na kwamba katika kipindi hicho vijiji 65 tu vilikuwa havina umeme.

“Mpaka kufikia Mei 2024 vijiji vilivyopata umeme vimeongezeka kutoka 489 mwezi Machi 2024 mpaka kufikia vijiji 538 mwezi Mei 2024 sawa na asilimia 97.1”’alisema Mhelela.

Naye Mhandisi wa TANESCO Mkoa wa Ruvuma Malibe Boniphace amevitaja vijiji 16 tu katika Mkoa ambavyo bado havipata huduma ya umeme.

Hata hivyo amesema wakandarasi wanaendelea na kazi ya kusambaza huduma ya umeme katika vijiji hivyo vilivyobaki.

Boniphace ameyataja wateja ambao wananufaika kupitia mradi wa REA tatu mzunguko wa pili katika Mkoa wa Ruvuma kuwa ni wateja 5214.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vijiji 554 na kati ya vijiji hivyo Tanesco imefanikiwa kufikisha huduma ya umeme katika vijiji 538 na kubakiwa na vijiji 16 Pekee.

## RC AFUNGUA MASOKO YA UFUTA,SOYA NA MBAAZI KUPITIA MFUMO



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amefungua masoko ya ufuta,soya na mbaazi kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na TMX wilayani Namtumbo.

Katika uzinduzi wa mnada wa kwanza mkoani Ruvuma katika zao la ufuta jumla ya kilo milioni 1,293,000 zimeuzwa kwa bei ya wastani wa shilingi 3,903 kwa kilo.

Akizungumza kwenye ufunguzi huo,Kanali Abbas amemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mfumo mzuri wa masoko ya mazao ya wakulima ambapo amesema mfumo huo unaleta manufaa makubwa kwa wakulima.

Amebainisha kuwa ,uendeshaji wa masoko ya zao la ufuta,mbaazi na soya hufanyika kupitia wakulima kununua,kusafirisha na kukusanya mazao kwenye

vyama vya msingi 101 vilivyopo katika wilaya za Namtumbo, Songea, Mbinga,Nyasa na Tunduru na vyama vikuu vya ushirika viwili ambavyo ni TAMCU na SONAMCU.

“Mfumo wa stakabadhi ghalani umedhibiti vipimo visivyo halali ambavyo vinamuibia mkulima kwa kuwa mfumo unatumia mizani ya kidijitali ambapo taarifa zote zinakuwa zimehifadhiwa’’,alisema.

Hata hivyo amekemea suala la utoroshaji wa mazao ambapo ameagiza serikali za mitaa kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa mazao na kuziagiza Halmashauri zihakikishe minada inaanza mapema kwa kuzingatia ratiba na kuweka usimamizi Madhubuti wa vyama vya ushirika katika shughuli zote zinazohusu mifumo ya masoko.

Mkuu wa Mkoa ameziagiza Halmashauri kuhakikisha zinatoa elimu ya mifumo ya masoko kwa wakulima na wadau wengine ambapo pia amewataka wanunuzi wa mazao na vyama vikuu vya ushirika kuhakikisha wanafanya malipo ya wakulima kwa wakati.

Naye Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Songea na Namtumbo (SONAMCU) Juma Mwanga ametaja hali ya masoko kwa mazao ya ufuta,soya na mbaazi kuwa inaridhisha ambapo katika kipindi cha miaka minne katika zao la ufuta jumla ya kilo 22,974,950 ziliuzwa na kuingiza Zaidi ya shilingi bilioni 59.

Amesema zao la soya katika kipindi cha miaka minne zimeuzwa kilo 12,915,722 na kuingiza Zaidi ya shilingi bilioni 13 na zao la mbaazi katika kipindi hicho zimeuzwa kilo 13,415,316 ambazo zimeingiza Zaidi ya shilingi bilioni 16.

Ameyataja baadhi ya mafanikio ya mazao mchanganyiko yaliyouzwa kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kuwa ni wakulima kupata bei nzuri ya mazao,kupungua kwa kiwango cha utoroshaji wa mazao,kuongezeka kwa wanunuzi na kuwepo ushirikiano baina ya wadau wa stakabadhi

## UZALISHAJI WA MAZAO RUVUMA WAFIKIA TANI MILIONI 1.8



UZALISHAJI wa mazao mkoani Ruvuma umeongezeka kutoka **tani 1,623,509.57 msimu wa mwaka 2020/2021** hadi kufikia **tani 1,823,509.57 katika msimu wa mwaka 2022/2023.**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema kuongeza kwa uzalishaji wa mazao hayo kumechangiwa na wakulima kuongeza matumizi ya mbolea ya ruzuku ambayo imeweza kuwafikia wananchi katika maeneo yao kwa gharama nafuu.

Amebainisha kuwa kutokana na serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea. matumizi ya Mbolea yameongezeka kutoka tani **50,524.50** msimu wa 2021/2022 hadi tani **93,955.7** msimu wa 2023/2024.

“Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya maboresho makubwa katika Sekta ya Kilimo kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya kilimo, mifumo ya ruzuku ya pembejeo na vyombo vya usafiri kwa Maafisa Ugani’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Amesema Serikali imetoa pikipiki **281** kwa maafisa ugani wote wa Kata na Vijiji kwa kwa Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuwawezesha Maafisa Ugani kuwafikia wakulima ili kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

Ameongeza kuwa serikali pia imetoa mashine **saba** za kupima afya ya udongo na kwamba Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi

yake ya TARI Uyole na Kampuni ya OCP iliwezesha upimaji wa Afya ya Udongo katika vijiji **100** vya Mkoa wa Ruvuma.

Ameongeza kuwa serikali imejenga maghala **31** yenye uwezo wa kuhifadhi tani **1,000** kila moja katika Halmashauri za Madaba ambako yamejengwa maghala 11, Halmashauri ya wilaya ya Songea maghala 12 na Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo yamejengwa maghala manane kupitia program ya ujenzi wa maghala kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka.

## WATUMISHI WA UMMA NYASA WAPATA MAFUNZO YA PEPMIS



Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetoa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma PEPMIS na PIPMIS kwa watumishi wa Umma wa Halmashauri na Taasisi za Serikali ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Mafunzo haya yamefanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Kilosa mjini Mbambabay.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watumishi wa Umma ili waweze kutoa Taarifa ya utekelezaji na kupimwa majukumu yao kupitia mfumo wa usimamizi wa utendaji kazi wa Utumishi wa Umma.

Akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi wa Idara na Sera na Mipango (ORMUUB) Bw Cyrus Kapinga amesema mafunzo haya ni muhimu kwa watumishi wa Umma kwa kuwa watakuwa wanatoa taarifa ya utendaji kazi na kupimwa kwa njia ya mfumo.

Amesema mafunzo hayo yatamwezesha mtumishi akiwa kwenye kituo chake cha kazi kutumia mfumo na mtumishi kuomba mikopo, uhamisho na shughuli nyingine nyingi.

Amesema Ofisi ya Utumishi imeamua kufika mikoani kwa ajili ya kufundisha na kufanya tathimini ya mfumo huu ili waweze kutatua changamoto zinazowakabili watumishi wanapotumia mifumo huo.

Ametoa rai kwa Watumishi kujifunza na kutumia mfumo huu kwa kuwa mfumo wa awali wa OPRAS ambao ulikuwa unapima utendaji kazi wa mtumishi wa umma umefutwa.

Awali akimkaribisha Mgeni rasmi kufungua mafunzo Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyasa Bw, Salum Ismail amewataka watumishi kufanya kazi kwa juhudi na kutoa taarifa ya utendaji kazi kupitia mfumo huu.

## TIMU YA TULIA TRUST YABISHA HODI RUVUMA




Timu ya Tulia Trust imewasili mkoani Ruvuma na kufanya mazungumzo na MKuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali. Ahmed Abbas Ahmed.

Timu hiyo imeweka kambi Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea kwa lengo la kuhakikisha wanaihudumia jamii ya watu wanao ishi kwenye mazingira magumu ili waweze kupata tabasamu kupitia mpango wa TULIA TRUST MTAANI KWETU.

Taasisi hiyo imefika mkoani Ruvuma mara baada ya kupokea maombi kutoka kwa wananchi wa Madaba pamoja na Mbunge wa Jimbo la Madaba Dkt.Joseph Kizito Mhagama baada ya kuonesha mwananchi anayeishi katika mazingira magumu ndani ya Jimbo la Madaba



# SERIKALI YATOA BILIONI 9.34 KUJENGA VITUO VYA AFYA 14 RUVUMA





Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 9.345 kujenga vituo vya afya 14 mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema fedha hizo zimetolewa kupitia fedha za mapato ya ndani, Tozo, Serikali Kuu na Wahisani.

Amesema vituo vyote vinajumuisha ujenzi wa majengo ya huduma ya mama na mtoto pamoja na majengo ya upasuaji.

Ameongeza kuwa serikali pia imejenga majengo manne ya huduma za dharura (EMD) Kwa gharama ya Zaidi ya Shilingi bilioni 1.5.

Ameyataja majengo ya EMD kuwa yamejengwa katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea,Hospitali ya wilaya ya Tunduru,Madaba na Nyasa na kwamba serikali imejenga jengo moja

la wagonjwa mahututi kwa gharama ya shilingi milioni 250 katika hospitali ya Halmashauri ya wilaya ya Mbinga.

Ameongeza kuwa serikali pia imetoa Zaidi ya shilingi milioni 152 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa,Serikali pia imetoa Zaidi ya shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea katika Kata ya Mwengemshindo Manispaa ya Songea.

Amesema Mkoa wa Ruvuma unaendelea na ukamilishaji wa Ujenzi wa zahanati 21 kwenye Halmashauri saba kwa gharama ya shilingi bilioni 1.05 na ukamilishaji wa Ujenzi wa Hospitali tano za Wilaya kwa gharama ya Shilingi Bilioni 3.4.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya mkoani Ruvuma,Kanali Abbas amesema hali imeendelea kuimarika, kwa kuwa upatikanaji umeongezeka kutoka asilimia 93 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 96 mwaka 2023.

Amesema Mkoa umepokea mashine ya CT scan na digital X-ray kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa na mashine ya X-Ray kwa ajili ya hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

## MBINGA MJI YATINGA KUMI BORA MASHINDANO YA USAFI



Halmashauri ya Mji wa Mbinga, mkoani Ruvuma imeshika nafasi ya 10 ya mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa ngazi ya miji nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa mashindano hayo yanayoratibiwa na Wizara ya Afya, Halmashauri ya Mji wa Mbinga kwa mwaka 2023 ilishika nafasi ya tisa kati ya Halmashauri za miji 21 zilizoshindanishwa nchini.

Katika nafasi hiyo, Mbinga Mji ilifungana na Halmashauri za miji ya Mbulu, Mkoa wa Manyara na Nanyamba,Mkoa wa Mtwara baada ya kupata asilimia 62 ya alama zote.

Halmshauri za miji zilizoitangulia Halmashauri ya Mbinga Mji ni Pamoja na Halmashauri za miji ya, Njombe asilimia kwenye mabano (89), Babati (73), Makambako (72), Nzega (71), Kibaha (70), Masasi (67), Mafinga (66) na Tunduma (64).

Halmashauri za miji zilizozidiwa na Halmashauri ya Mji Mbinga na asilimia zake kwenye mabano Halmashauri za miji Kasulu (56), Geita (56), Newala (56), Handeni (52), Ifakara (52), Tarime (46), Korogwe (46), Bunda (45), Bariadi (44) na Kondoa (30).

Akizungumza ofisini,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Bi. Amina Seif amewapongeza wakazi wa Mbinga Mji na wadau wengine kwa jitihada zao za kulivaa jukumu la usafi wa mazingira yao.

Afisa Afya wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Bw. Felix Matembo amesema mafanikio waliyoyapata ni chachu kwa Mbinga Mji kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya mwaka 2024.



# RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA MIUNDOMBINU RUVUMA




Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarishaji miundombinu katika Mkoa wa Ruvuma

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ameitaja baadhi ya miundombinu hiyo kuwa ni Pamoja na upanuzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege Songea kimekarabatiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 37.

Miundombinu mingine ameitaja kuwa ni ujenzi wa soko katika kijiji cha Peramiho wilayani Songea unaendelea kwa gharama ya Zaidi ya shilingi milioni 200.7 na ujenzi wa kituo cha mabasi katika kijiji cha Parangu unaendelea kwa gharama ya Zaidi ya shilingi miliobi 225.

Kulingana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Serikali pia imejenga Bandari kubwa na ya kisasa ya Ndumbi katika ziwa Nyasa kwa gharama ya bilioni 12.5 .

Amebainisha kuwa Bandari hiyo ina gati lenye urefu mita 160 kwenda ziwani, urefu (jetty head) wa mita 20.4, ramp urefu wa kwenda Ziwani mita 40 urefu (Ramp head) mita 10, ghala la kuhidhi mizigo inayoathiriwa na mvua lenye mita za ukubwa 2,020, eneo lenye sakafu ngumu (heavy heavy yard) kwa ajili kuhifadhi mizigo isiyoathiriwa na mvua lenye ukubwa wa meta za mraba 9,030 na jengo la kupumzikia abiria na ofisi na nyumba za watumishi.

Amesema serikali pia inatarajia kujenga Bandari mpya ya kisasa ya Mbamba Bay kwa lengo la kuimarisha Ushoroba wa Maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor), ambayo ni njia fupi na rahisi ya kuhudumia mzigo wa Malawi kutokea Bandari ya Mtwara.

Amesema bandari hiyo inaunganishwa kwa barabara hadi Bandari ya Mbamba Bay na kuunganisha hadi Bandari za Malawi kupitia majini.

Hata hivyo amesema Ili kutekeleza mradi huo mkubwa, Serikali ya Awamu ya sita imetoa Zaidi ya shilingi bilioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari kubwa na kisasa ya Mbamba Bay.

## UZALISHAJI PARACHICHI MBINGA WAFIKIA ASILIMIA 400



Uzalishaji wa zao la parachichi katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga mkoani Ruvuma umepaa kwa asilimia 400 katika kipindi cha miaka mitatu.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga Bw. Enock Ndunguru amesema uzalishaji wa zao hilo umeongezeka mpaka kufikia

tani 40 katika msimu wa mavuno wa mwaka 2023 ambayo ni sawa na ongezeko la tani 32 ikilinganishwa na tani nane zilizozalishwa mwaka 2021.

Amesema ongezeko hilo limechangiwa na mazingira rafiki yaliyotengenezwa na serikali kwa lengo la kuvutia wakulima kujikita zaidi katika kilimo cha parachichi.

“Eneo la uzalishaji wa zao la parachichi katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga limeongezeka kutoka hekari 80 mwaka 2021 hadi kufikia hekari 182 za sasa, hii inatia moyo kwa hakika”, alisisitiza Ndunguru.

Amesema zao la parachichi licha ya kuwa chanzo cha kipato, lakini pia parachichi ni  zao rafiki wa mazingira.

Parachichi, kitaalamu linaitwa Persea Americana ni tunda lenye virutubisho muhimu sana vinavyohitajika katika mwili wa binadamu na linaongeza kipato kwa familia na Taifa

## TAMCU YAPATA VIONGOZI WAPYA WA BODI,DC TUNDURU ATOA MAAGIZO



Chama Kikuu cha Ushirika wa Masoko ya Mazao Tunduru (TAMCU LTD) kimefanya Mkutano Mkuu uliokwenda sanjari na Uchaguzi wa kupata Bodi mpya ya Uongozi wa chama hicho.

Viongozi waliochaguliwa kwenye mkutano huo ni Pamoja na Ndg. Mussa Athumani Manjaule ambaye amechaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Bodi mpya ya TAMCU, Bodi ambayo inaundwa na wajumbe sita.

Mkutano huo ulifanyika mjini Tunduru na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, viongozi wa vyama vya ushirika, na wanachama wa TAMCU kutoka vyama vya Ushirika vya Msingi vyote vilivyopo wilayani humo.

Mgeni rasmi kwenye mkutano huo alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Mhe. Simon Chacha.

Akizungumza kwenye mkutano huo Chacha amewataka viongozi wapya wa TAMCU kusimamia kwa ufanisi mambo na mikakati waliyoahidi kwa wanachama wao.

Amesisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi na wanachama, na akawataka wanachama kuchagua viongozi waadilifu watakaowezesha ushirika kufikia maendeleo endelevu.

“Maendeleo ya Ushirika yanahitaji ushirikiano,uadilifu na uaminifu, hivi vyote vinatakiwa kuanza kutengenezwa na sisi viongozi wenyewe’’,alisema Chacha.

Mwenyekiti mpya akizungumza baada ya kuchaguliwa Ndg. Manjaule ameshukuru wanachama kwa kumwamini tena kuwa kiongozi wao,ambapo ameahidi kutekeleza mikakati yote ya TAMCU kwa lengo la kuimarisha ushirika na kuleta maendeleo kwa wanachama wake.

Mkutano huo pia umeshuhudia uzinduzi wa magari mawili mapya ya mizigo aina ya Scania yaliyonunuliwa na vyama vya ushirika vya msingi vya SAMA AMCOS na NGUVUMALI AMCOS kwa ushirikiano na benki ya CRDB.

Magari hayo yananatarajiwa kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wakulima kutoka vijijini.

# MADABA WAPONGEZWA KWA KUFANYA VIZURI MITIHANI YA TAIFA



Afisa Elimu Awali na msingi katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma Mwl. Saada Chwaya amewapongeza walimu na kuwakabidhi zawadi mbalimbali kwa kuiwezesha Halmashauri hiyo kushika nafasi ya kwanza Kimkoa katika mitihani ya Taifa ya darasa la saba na darasa la nne mwaka 2023.

Chwaya ametoa Pongezi hizo katika kikao cha tathmini kilichoambatana na sherehe za kuwakabidhi zawada walimu na wanafunzi waliofanya vizuri zilizofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri hiyo mjini Madaba.

“Nilijisikia faraja sana katika kikao cha Maafisa Elimu wa Halmashauri 184 wa Nchi nzima na mikoa 26,baada ya Halmashauri yetu kufaulisha kwa wastani wa asilimia 85, Katibu Mkuu wa TAMISEMI alitupatia zawadi ya cheti nikiwemo mimi nawashukuru sana walimu wangu”,alisisitiza.

Afisa Elimu huyo ametoa rai kwa walimu hao kuendeleza wimbi la kufaulisha wanafunzi kwa mwaka huu ili kuendelea kupeperusha bendera ya Mkoa wa Ruvuma kitaaluma.

# DED SONGEA AAGIZA KUONGEZA KASI UTEKELEZAJI MIRADI



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya mkoani Ruvuma Songea Bi. Elizabeth Mathias Gumbo amewataka mafundi kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili iweze kukamilika kwa wakati .

Gumbo ametoa maagizo hayo baada ya kukagua ujenzi Miradi saba inayotekelezwa katika Halmashauri hiyo.

“ Tupo nyuma ya muda, tunayo pesa ya kutosha hivyo kwa wale wote wanaosimamia miradi hakikisheni mnashinda site na kusimamia mafundi muda wote”, alisema Gumbo.

Miradi iliyokaguliwa na Mkurugenzi huyo ni pamoja na Shule ya Sekondari Maposeni ambapo alikagua Ujenzi wa jengo la utawala lililotengewa Zaidi ya shilingi milioni 74, Ujenzi wa Madarasa 17 yenye thamani ya Zaidi ya Shilingi 408 na Matundu 25 ya vyoo yenye thamani ya Zaidi ya 44.

Miradi mingine aliyaikagua ni madarasa 10 katika Shule ya Sekondari Jenista Mhagama, alipita na kukagua ujenzi wa Madarasa kumi yenye ya shilingi milioni 240 na Matundu ya Vyoo 19 yenye thamani ya Shilingi milioni 33.

## RC RUVUMA ATAHADHARISHA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZISIZOZINGATIA SHERIA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed ametahadharisha kuwa shughuli za kiuchumi zisipofanywa kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam zinaweza kuharibu mazingira na kutishia mustakabali wa Maisha ya viumbehai.

Kanali Abbas ametoa tahadhari hiyo wakati anazungumza kwenye maadhimisho ya siku ya Uhuru wa vyombo vya Habari Duniani ambazo kimkoa zimefanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na wadau wa Habari na na wanahabari.

“Kuna uchimbaji wa madini unafanyika kwa mtazamo ni shughuli ya kiuchumi kama isipofanywa vizuri kwa kuzingatia sheria,kanuni na ushauri wa kitalaam,unaweza kugeuka uchumi wenye kuharibu mustakabari wa maisha ya watu’’,alisisitiza.

Amesema kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema uandishi wa Habari na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi,inakwenda kuugusa muhimili wa Habari ili wanahabari wakafanye kazi ya kuhabarisha umma kuhusu madhara yanayoweza kutokea kwa kutozingatia kanuni na sheria za uendeshaji wa shughuli za kiuchumi hivyo kusababisha mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa.

Amesema Rais Dkt.Samia amefanya kazi kubwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambapo ameweza kuanzisha mikakati na program mbalimbali ili

kuhakikisha taifa na Dunia inaendelea kuwa salama kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Amebainisha kuwa hivi karibuni Rais Samia amezindua mkakati wa nishati safi ikiwa ni sehemu ya uendelezaji wa kampeni za kupambana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa.

Amesema madhara yameanza kujitokeza ambapo hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la joto kwenye uso wa dunia,pia kumekuwa na uyeyushaji wa barafu kwenye bahari na kusababisha ongezeko la maji ambalo pia limesababisha madhara mengi ikiwemo elnino na lanina.

Ameongeza kuwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kumetokea madhara mbalimbali kama vimbunga ambapo hivi karibuni kimetokea kimbunga Hidaya ambacho kimeleta madhara makubwa.

Amesema madhara ya mabadiliko ya tabianchi ni mengi na kwamba yasipoelezwa vizuri kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari, wananchi wanaweza kuendelea kufanya shughuli za kiuchumi bila kufuata kanuni na sheria,hivyo amesisitiza kuyatunza mazingira ili Taifa liendelee kuwa salama.

Akizungumzia maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya Habari Duniani,Kanali Abbas amewapongeza wanahabari kwa kufanya kazi nzuri ya kuhabarisha umma kazi mbalimbali zinazofanyika na serikali ndani ya Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla.

Hata hivyo ametahadharisha kuwa wakati wanahabari wanatekeleza majukumu yao,wasiache kuangalia utekelezaji wa 4R za Mheshimiwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Ameahidi serikali ya Mkoa wa Ruvuma ipo tayari kushirikiana na wanahabari na kwamba yupo tayari kutoa kila aina ya ushirikiano unaohitajika ili kuhakikisha kazi ya wanahabari inakuwa nyepesi na matakwa ya muhimili wa kuhabarisha umma haukwami.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile amesema katika Tanzania sheria zinawapa heshima kubwa waandishi wa Habari na kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoheshimu uhuru wa Habari.

Ndile amesisitiza kuwa huwezi kuheshimu vyombo vya Habari bila kuheshimu wanahabari wenyewe ambapo amesema wanahabari wamefanyakazi kubwa iliyotuka katika wilaya ya Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Ruvuma Amon Mtega amempongeza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuyaunganisha makundi mbalimbali wakiwemo wanahabari .

## SHIRIKA LA BRITEN LATOA ELIMU YA VIUATILIFU KWA WAKULIMA MADABA




Shirika la BRITEN ambalo linajihusisha na utoaji wa elimu ya kilimo kuhusu Pembejeo na mbegu bora limetoa elimu ya matumizi bora ya viuatilifu kwa wakulima wa Halmashauri ya Madaba Wilayani Songea mkoani Ruvuma.

BRITEN imetoa elimu hiyo kupitia mashamba darasa ya mazao mbalimbali ikiwemo zao la mahindi na maharage.

Akizungumza katika mkutano Afisa Kilimo wa BRITEN Elly Nyava amewashauri wakulima wa Mkoa wa Ruvuma kutokata tamaa katika kilimo badala yake wajikite Zaidi katika Uzalishaji wa kilimo chenye tija.

Nyava amewashauri wakulima wa Mkoa wa Ruvuma kuendelea kutumia majukawaa mbalimbali yanayotoa elimu ya kilimo Pamoja na kufuata ushauri wa mabwana shamba na wataalamu wa kilimo ili kuongeza uzalishaji.

Kwa upande wake Kiongozi Ufuatiliaji wa Miradi Rehema Selemani ameitaja faida ya matumizi sahihi ya Mizani ya kidigitali inavyomwezesha mkulima kujua Ujazo wa mazao yake baada ya kuuza mazao hayo.

## DED MBINGA AWAFUNDA WANAFUNZI KUZINGATIA MASOMO



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma Joseph Rwiza amewataka wanafunzi wote kuzingatia masomo na kutambua jitihada zinazofanywa na wazazi wao za kuhakikisha wanapata elimu bora.

Amewataka wanafunzi hao kutambua azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuimarisha na kuboresha sekta ya elimu nchini.

Rwiza ametoa wito huo alipozungumza na wanafunzi wa shule za Sekondari Ruanda na Litumbandyosi katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

" Nafasi hii mlioipata itumieni vizuri wazazi wanataka mpate elimu bora lakini pia Rais wetu amewekeza fedha nyingi ili tujifunze katika mazingira rafiki" Amebainisha Rwiza

## BODI YA VETA YAFANYA ZIARA MKOANI RUVUMA



Pichani ni Mkuu wa mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas akizungumza na Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Prof. Sifuni Mchome ambapo ameambatana na Mkurugenzi Mkuu wa VETA nchini C.T.A Anton Kasole na Wajumbe mbalimbali wa Bodi ya VETA.



# RC ABBAS AWAPONGEZA WASANII WA NYOTA YA RUVUMA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amekipongeza kikundi cha sanaa cha Nyota ya Ruvuma kilichopo wilayani Namtumbo ambacho kilitoa burudani ya kupendeza kwenye maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia duniani ambazo kimkoa zimefanyika kijiji cha Suluti wilayani Namtumbo na kuhudhuriwa na wawakilishi kutoka wilaya zote tano za Mkoa wa Ruvuma



# FORVAC WAKABIDHI MASHINE YA KISASA KUCHAKATA MAGOGO SONGEA



Program ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC) kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imekabidhiwa mashine ya kisasa inayotembea kwa ajili ya kuchakata mbao ili kuendeleza Usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Mratibu wa FORVAC Mkoa wa Ruvuma Petro Masolwa amemkabidhi mashine hiyo Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile katika hafla iliyofanyika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Songea



# SERIKALI KUTOA MAAMUZI SOKO LA MADINI YA VITO TUNDURU




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema ndani ya siku saba kuanzia Mei 15,2024,serikali itatoa maamuzi ya uwepo wa soko moja au masoko matatu ya madini ya vito wilayani Tunduru.

Akizungumza na wanahabari ofisini kwake mjini Songea,Kanali Abbas amesema akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Tunduru hivi karibuni aliweza kutembelea masoko ya madini ya vito ambayo ni soko la Generation,TUDECU na kukagua ujenzi wa soko jipya la madini.

Amesema akiwa katika masoko ya madini ya Generation na TUDECU walijitokeza wananchi wengi ambao walitaka kupata ufafanuzi wa baadhi ya kero zinazowasumbua ambapo baadhi ya wananchi walijitambulisha kuwa ni wafanya biashara wa madini ya vito wilayani Tunduru.

Amesema wafanyabiashara hao waliiomba serikali kuwatafutia fursa za mikopo kwenye Taasisi za fedha ili waweze kufanya biashara za madini kwa ufanisi mkubwa.

Ameongeza kuwa wafanyabiashara hao pia walikuwa na hoja ya kutaka majibu ya serikali ni juu ya uwepo wa masoko Zaidi ya moja ya uuzaji wa madini ya vito wilayani humo.

“Kwa ugeni wangu niliona masuala haya hayahitaji majibu ya haraka,niliwashauri wanipe muda ili niweze kuwapatia majibu,leo nimewaita wanahabari kuwajulisha kwamba,jambo hilo serikali inalifanyia kazi kwa kuwa ni jambo linalohitaji utafiti mkubwa na majibu mazuri’’,alisisitiza Kanali Abbas.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Mkoa amesema aliamua kuunda Tume maalum ya wataalam ambayo itakwenda kufanya utafiti wa hoja zote hizo ili majibu yatakayorudi yaweze kutoa maamuzi ya serikali juu ya uwepo wa soko moja au masoko matatu ya madini wilayani Tunduru.

Amesisitiza kuwa msimamo wa serikali utatolewa baada ya timu hiyo maalum kukamilisha kazi yake na kuleta majibu ndani ya siku saba.

Wilaya ya Tunduru ina utajiri wa karibu aina zote za madini ya vito isipokuwa madini ya tanzanite ambayo katika dunia nzima yanapatikana Mirerani mkoani Manyara.



## RC RUVUMA ASIKITISHWA NA HALI YA MALEZI YA WATOTO




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesikitishwa na hali isiyoridhisha ya malezi na uangalizi wa mtoto.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia ambayo kimkoa yamefanyika Kijiji cha Suluti wilayani Namtumbo,amesema wazazi na walezi wengi wamekuwa hawatimizi ipasavyo majukumu ya malezi na kusababisha malezi ya upande mmoja.

"Takwimu kutoka ofisi ya Ustawi wa Jamii Mkoa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2023 zinaonesha kuwa jumla ya mashauri 3,441 yalipokelewa na kushughulikiwa ambapo mashauri 1,611 sawa na asilimia 47 yalihusu matunzo ya watoto,mashauri 831 sawa na asilimia 24 yalihusu matatizo ya ndoa na mashauri 969 sawa na asilimia 29 yalihusu mashauri nje ya ndoa'',alisema Kanali Abbas.

Amebainisha kuwa Ofisi ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikipokea kesi za matunzo ya Watoto na malalamiko yanayoelekezwa upande wa akinababa.

Ametoa rai kwa wazazi na walezi ambao wamefarakana kutambua kuwa mtoto bado anastahili malezi yaliyo bora hivyo ni vema kuweka mpango mzuri wa kumlea mtoto ili asiathirike kimalezi na kwamba wazazi wajitahidi kuvumiliana ili kuepusha kuachana kusiko kwa lazima hivyo kumuathiri mtoto.

Akisoma risala ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya familia Mariam Juma ambaye ni Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

ameitaja kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema tukubali tofauti zetu kwenye familia,kuimarisha malezi ya Watoto, inawakumbusha wazazi na walezi kuweka kando tofauti zao na kuangalia malezi na huduma zinazostahili kwenye familia.

Juma amebainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2023 mashauri 2,859 ya ukatili yalitolewa taarifa na kushughulikiwa katika ofisi za ustawi wa Jamii Mkoa wa Ruvuma na kwamba mashauri 121 yalifikishwa mahakamani.

Hata hivyo amesema mashauri 77 sawa na asilimia 63.6 yalihukumiwa,kati ya mashauri 1,580 ya Watoto,mashauri 1050 sawa na asilimia 66.6 yaliwahusu wasichana wakati mashauri 1,279 ya watu wazima,mashauri 1,030 sawa asilimia 80.5 yaliwahusu wanawake.



## WAGONJWA 568 WAPATA HUDUMA ZA KIBINGWA MADABA




WAGONJWA 568 wa Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma wamepata huduma na kutibiwa na Madaktari bingwa walioletwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt .Samia Suluhu Hassan .

Madaktari hao walianza kazi katika Mkoa wa Ruvuma Mei 6,2024 na wamehitimisha zoezi hilo Mei 10 katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Madaba Dr.Chacha Wambura amesema ujio wa Madaktari hao umesababisha upatikanaji wa fedha zaidi ya shilingi Milioni mbili kwa wagonjwa waliopata matibabu bila bima.

Hata hivyo Wambura amemshukuru Rais Samia kwa kuleta Madaktari bingwa ambao wameleta chachu kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kupata huduma na kwa upande wao Madaktari wamejifunza mambo mengi.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo Mussa Rashid amesema kupitia zoezi la Madaktari bingwa wamejipanga kuhakikisha wanaboresha utoaji wa huduma za Afya katika hospitali hiyo ambayo pia inapokea wagonjwa wengi kutoka Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe

# LUTENI KANALI MSTAAFU ALIYESOMA NA ID AMIN ALIVYOZIKWA KIJESHI SONGEA



Luteni Kanali Mstaafu Daniel Gangisa ambaye alisoma na Dikteta Idd Amini wa Uganda kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 1952 hadi 1955 amezikwa kijeshi nyumbani kwake Chandarua Manispaa ya Songea



# RUVUMA WALIVYOADHIMISHA SIKU YA MAMA DUNIANI



Mke wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Bi. Riziki Suleiman Nkya amewaongoza akimama wa Mkoa wa Ruvuma kuadhimisha siku ya mama Duniani katika hafla aliyowaandalia akina mama wa Mkoa wa Ruvuma.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Chandamali mjini Songea alikuwa ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma ndugu Rehema Sefu Madenge.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Bi. Riziki amewaasa akina mama kuzilea familia zao katika malezi bora kwa sababu wao ndiyo nguzo ya maendeleo ya familia.

Amewasisitiza akinamama hao kuishi katika maadili mema na kuwa mfano bora katika jamii inayowazunguka.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Rehema Madenge akizungumza kwenye hafla hiyo amesema kuelekea katika siku ya familia Duniani ambayo kilele chake ni Mei 15 mwaka huu amewaasa akina mama kutumia siku hiyo kujitafakari kama wanatimiza wajibu wao kama akina mama katika familia.

## MBUNGE NYASA ATOA KILO 500 ZA MCHELE LITUHI



Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya amekabidhi chakula kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokea hivi karibuni katika Kata ya Lituhi wilayani Nyasa

Makabidhiano yamefanywa na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyasa shanel Mbunda, katika viwanja vya Ofisi ya Afisa Mtendaji Kijiji Cha Kihuru Kata ya Lituhi.

Akikabidhi chakula hicho kwa waathirika wa mafuriko, amesema ametumwa na Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya kuwapa pole na kuwakabidhi chakula, baada ya mafuriko kubomoa nyumba za wakazi wa Lituhi, na baadhi ya mashamba kuharibika.

Msaada uliotolewa na Mbunge huyo ni mchele kilo 500 ambao umetolewa kwa waathirika 45 katika kaya 12.

Wakipokea chakula, wananchi wa Kata ya Lituhi wamemshukuru na kumpongeza Mbunge kwa Kwa msaada aliyoutoa.

# DC TUNDURU AWAAGIZA USIMAMIZI CHAKULA SHULENI



Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Mheshimiwa Simon Kemori Chacha, amewaagiza viongozi katika kata na vijiji, pamoja na maafisa elimu kata kuhakikisha wananfunzi wanapata mlo wakiwa shuleni wakati wa masomo.

Amesema kuwa kufanya hivi kutaongeza ufanisi na umakini kwa wanafunzi katika masuala ya elimu, hasa katika kuongeza uelewa pale wanapofundishwa na walimu wao.

"Lishe ni kitu muhimu sana katika maisha ya kila mwanadamu , tunatakiwa kulichukulia hili suala kwa uzito wake katika maeneo yetu tunayoishi".Alisema Chacha.

Chacha  ametoa agizo hili wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa afua za lishe ngazi ya wilaya. Kikao hicho kilihudhuriwa na watendaji wa kata pamoja na wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Mkuu wa Wilaya amesisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi wa kata na vijiji, maafisa elimu, na jamii kwa ujumla katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mlo bora shuleni. Alisema kuwa ushirikiano huo utasaidia kufanya kazi ya kuendeleza lishe bora katika Wilaya ya Tunduru.

# WANAFUNZI MADABA KUPIMWA VIWANGO VYA UONI NA USIKIVU




Wanafunzi wa darasa la awali hadi darasa la nne katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma wanatarajia kuanza kupimwa viwango vyao vya uoni na usikivu kuanzia Mei 13 hadi 19, 2024.

Akizungumza katika kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Afisa Elimu Msingi Saada Chwaya amesema Ofisi ya Rais TAMISEMI imepanga kufanya zoezi hilo litafanyika katika Mikoa minne ambayo ni Ruvuma, Mtwara,Mbeya na Iringa ili kubaini wanafunzi wenye changamoto ya kuona na kusikia.

Kwa upande wake mratibu wa Jifunze uelewe Mkoa wa Ruvuma amesema wanafunzi watakaogundulika kuwa na changamoto za uoni na usikivu watachunguzwa zaidi kitaalam na kupatiwa afua stahiki vikiwemo visaidizi kama vile miwani na shimesikio.

# DAS SONGEA ATAJA UMUHIMU WA CHAKULA KWA WANAFUNZI



Katibu Tawala wa Wilaya ya Songea  Mtela Mwampamba, amewaagiza watendaji wa Kata na Wakuu wa Shule wote kuhakikisha  kila Mzazi anachangia gharama za chakula ili kumhakikishia mtoto kupata chakula .

Mwampamba ameyasema hayo katika kikao cha Kamati ya Lishe kilichofanyika katika ukumbi wa Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea yaliyopo Lundusi Songea.

Kikao hicho ambacho huratibiwa na Divisheni ya Afya, kimeshirikisha watendaji wa kata zote 16 za Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Katibu Tawala huyo amewaagiza watendaji wa Kata na Kijiji kuhakikisha wazazi wote wanachanga chakula kwa ajili ya Watoto wao.

Amesisitiza elimu ya lishe bora na ulaji iendelee kutolewa kwa jamii kupitia Mikutano yote ya Hadhara, Makongamano, Semina na Mashuleni pamoja na  kupitia vyombo vya Habari.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**



**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**

**KUPITIA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**


S.L.P 74 SONGEA

57180 RUVUMA

SIMU NAMBARI.025- 2602256 / 2602238

FAX NA.2602144

E-MAIL: RAS.RUVUMA@TAMISEMI.GO.TZ

TOVUTI:WWW.RUVUMA.GO.TZ

INSTAGRAM; RS RUVUMA

FACEBOOK: RS RUVUMA

YOUTUBE:RS RUVUMA


***www.ruvuma.go.tz***